





Katika kijiji kimoja,  
kulikuwa na mvulana  
aliyeitwa Abula.

Abula hakupenda kusoma  
wala hata kufungua  
kitabu. Licha ya kuwa  
mwanafunzi mvivu  
alikuwa na tabia mbaya.



Abula alizoea kuiba pesa za mamake na kununua peremende. Hata mama alipozificha, Abula alizipata.

Alipomaliza kula peremende, Abula angeenda kucheza na marafiki zake.



Baada ya muda, Abula  
aliacha kwenda shulen.  
Alicheza mchana kutwa na  
kurudi nyumbani jioni.

Mamake alipogundua  
jambo hilo, alikuwa na  
wasiwasi.




Mama alimwambia  
mumewe, "Mtoto wetu  
amekuwa mtukutu.  
Nadhani hata haendi  
shuleni. Pia ananiibia  
pesa."

Baba aliwaza juu ya njia  
mwafaka ya kubadilisha  
tabia za Abula.



Alimwambia mkewe,  
“Wakati mwingine, zifiche  
pesa zako katika kurasa za  
kitabu. Kwa vile yeye  
hafungui vitabu, pesa  
zako zitakuwa salama  
pale.”



Siku iliyofuata, Abula  
alitafuta pesa za mamake  
kila mahali lakini  
hakupata chochote.

Aliamua kwenda soko  
iliyokuwa karibu kuona  
kama angepata pesa  
zozote.




Baba aliona kule Abula  
alikuwa akienda.

Alisema, "Mwanangu,  
ninajua kwa nini  
unakwenda sokoni. Sasa  
rudi nyumbani ukatafute  
pesa kwenye vitabu."



Abula alishangaa, lakini  
alikwenda nyumbani  
akatafuta kwenye vitabu.

Alizipata pesa ambazo  
mamake alikuwa  
ameficha.



Siku iliyofuata, Abula alitafuta tena kwenye vitabu. Lakini, hakuna pesa zozote zilizokuwa zimefichwa humo.

Alimwuliza babake kwa nini hakupata pesa zozote kwenye vitabu.



Babake alitabasamu kisha akamjibu, "Mwanangu, je, ungependa upate pesa nyingi za kununua vitu vingi vitamu?"

Abula alimjibu, "Bila shaka, baba."



Babake alisema, "Nisikilize vizuri. Soma vitabu vyako na uhudhurie shule. Utapata zawadi nyingi kwenye vitabu. Usikate tamaa."

Abula alijibu, "Lakini baba, kusoma ni kazi ngumu. Vitabu vinachosha mno!"



Baba aliwaza juu ya  
kumhamasisha mwanawe.  
Alimwambia Abula, "Hebu  
tusome pamoja.  
Nitakusaidia upate mali  
vitabuni."

Abula alisoma kwa bidii.  
Mwishoni, alifaulu na  
kuishi maisha mazuri.